JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

CHUO CHA UALIMU MHONDA

S L P 14 TURIANI MOROGORO

MKUU WA CHUO: +255784 454463

MAKAMU MKUU WA CHUO: +255 7134 68781

OFISI YA USAJILI: +255763589385, +255784595836, 0756841024

BARUAPEPE:mhondatc@moe.go.tz
TOVUTI:www.mhondatc.ac.tz

KUMB.NA.MH/CCU/70/JOIN/2023 **TAREHE 10/06/2023**

MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU

MWAKA 2023/2024

1. UTANGULIZI

Tunafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi/Awali kwa mwaka wa masomo 2023/2024. Hii ni nafasi ya pekee kwako kwani wengi hawakubahatika kuipata. Chuo kinaendesha Mafunzo ya **Astashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi** na **Astashahada ya Ualimu Elimu ya Awali** kwa muda wa miaka **miwili (2**). Ni matumaini yetu kwamba ufikapo hapa Chuoni utaitumia fursa hii vizuri.

Chuo cha Ualimu Mhonda kipo katika Mkoa wa Morogoro, Wilaya ya Mvomero, Tarafa ya Turiani, kata ya Mhonda, kijiji cha Mhonda. Ni umbali wa kilometa 104 kutoka Stendi ya Msamvu iliyopo Morogoro mjini, na kilometa 3½ kutoka Turiani kituo cha mabasi Mapate hadi Chuoni.

2. NAMNA YA KUFIKA CHUONI

2.1. Ufikapo kituo cha Mabasi Morogoro (Msamvu), Panda NOAH zinazoelekea Turiani. Pia yapo mabasi ambayo ni; BM COACH, ZENJIBAR, KVC, MSUYA na ZEELAND, N.k. Nauli yake ni Tsh. 7,000/= tu. Kwa wale wanaotokea mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga panda Mabasi yafuatayo; MAPENZI YA MUNGU, KVC na SIMBA MTOTO shuka katika kituo cha mabasi **Mapate** Turiani.

2.2. Ufikapo Turiani shuka katika kituo cha Mapate, chukua usafiri kuelekea Chuoni. Nauli ya pikipiki ni Tsh 2,000/= tu. **NB:** Unashauriwa kufika Chuoni mapema kabla ya saa 12.00 jioni.

3. KUSAJILIWA CHUONI

Mara ufikapo Chuoni pitia hatua zifuatazo ili kukamilisha usajili wako:

3.1. Onana na mlinzi ili upate maelekezo

3.2. Onana na Msajili wa Wanachuo ili uwasilishe Vyeti Halisi, Result Slip na nakala zake. Vyeti hivyo ni;

3.2.1. Cheti cha kidato cha nne kwa wahitimu wa nyuma ya 2022 AU Result Slip kwa wahitimu wa 2023.

3.2.2. Cheti cha kidato cha Sita kwa wahitimu wa nyuma 2022 au Result Slip kwa wahitimu wa 2023.

3.2.3. Vyeti vya kuhitimu Shule (School Leaving Certificates- kama unacho)

3.2.4. Cheti cha kuzaliwa.

3.2.5. Cheti cha ndoa (Kwa aliyeoa/aliyeolewa)

3.2.6. Onana na Mhasibu wa Chuo ili ukabidhi risiti za Ada na Michango uliyolipia Benki.

3.2.7. Onana na Boharia ili kukabidhi vifaa/Rim ya karatasi A4

3.2.8. Onana na Mratibu Taaluma ili upangiwe darasa.

3.2.9. Onana na Mwadili wa wanachuo ukaguliwe vifaa na upangiwe bweni.

NB: Chuo hakitampokea na kumsajili Mwanachuo;

3.2.9.1. Atakayekuja bila vyeti halisi (**Originals**). Aidha, kwa yeyote atayewasilisha vyeti visivyo halali hatua zitachukuliwa dhidi yake ikiwa ni pamoja na kupelekwa kwenye vyombo vya kisheria.

3.2.9.2. Atakayekuwa hajakamilisha malipo ya Ada na Michango. Aidha, kwa wale wanaofadhiliwa na mashirika waje na vithibitisho vyao vyenye saini na muhuri wa shirika/idara husika.

3.2.9.3 . Atakayekuwa hana kadi ya Bima ya afya ya NHIF au fedha ya kukatia Bima Tsh 50,400/=

4. MAHITAJI MUHIMU KWA WANACHUO

4.1. **SARE**: Wavulana na Wasichana waje na mashati 2 ya mikono mirefu ya bluubahari na tai ndefu nyeusi. Mashati yawe marefu ili uweze kuchomekea vizuri yanapovaliwa.

4.2. Wavulana waje na Suruali nyeusi 2 zenye marinda (Cerebration) na mifuko mitatu, iwe ndefu kugusa kiatu na upana chini iwe inchi 16 na mkanda mweusi wa ngozi wenye Bakozi ya saizi ya kati (Angalia picha) kwenye tovuti ya chuo **www.mhondatc.ac.tz**

4.3. Wasichana washone sketi 2 nyeusi kwa kutumia kitambaa cha suti, ziwe sketi za linda box mbele tu na ndefu za kuvuka magoti. Watakaotumia hijabu washone sketi nyeusi, shati/nusu kanzu na juba (vyote viwe vya bluubahari).

4.4. Koti la suti nyeusi linaloendana na suruali au sketi.

4.5. Unatakiwa kuwa na mavazi yasiyozidi **matano (05)** yenye heshima na hadhi yatakayotumika baada ya vipindi vya darasani. NB: Nguo za kubana, fupi,

zinazoangaza, mipasuo kupita magoti, pensi nyanya, timberland, jeans na nyingine za aina hiyo haziruhusiwi Chuoni. Unatakiwa kuja na **begi dogo** la kuhifadhia vifaa na nguo zako.

4.6. Uwe na viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi vya kutumbukiza kwa jinsi zote (Me/Ke). Soksi jozi 2 au zaidi **nyeupe** kwa wasichana na **nyeusi** kwa wavulana.

4.7. Uje na Nguo za michezo: (a) Bukta za **blue** kwa wanaume na Sketi za solo rangi ya **dark blue** kwa Wasichana. (b) Tracksuit zenye michirizi mweupe (Wavulana iwe ya rangi **nyeusi** na Wasichana iwe ya rangi ya **njano**. (c) Viatu/ Raba za michezo.

4.8. Aje na **T-Shirt moja** rangi ya **njano** yenye kora (Form Six). NB: Tembelea tovuti ya chuo **www.mhondatc.ac.tz** kuona sampuli ya **Sare zote** za chuo.

4.9. Shuka nne au zaidi mbili ziwe za bluu bahari kwa wavulana **na wasicha waje na shuka nne au zaidi, mbili ziwe za rangi ya Pink yasiwe na Urembo wowote**, mto na foronya nyeupe, Chandarua cheupe cha pembe nne chenye ukubwa wa futi nne kwa sita (ft4x6) kwani eneo hili lina mbu wengi.

4.10. File folder 2 kwa ajili ya kuwekea kumbukumbu binafsi na Rimu mbili (2) za Karatasi za A4, moja ya chuo na nyingine kwa matumizi yako binafsi.

4.11. Mathematical set, daftari kubwa 14 (Counter Book Quire Two Au Three) za kuanzia, rula ya futi moja, Kalamu na penseli za kutosha.

4.12. Aje na kadi ya bima ya afya NHIF na kama huna njoo na Tsh 50,400/=.

5. VIFAA BINAFSI

Vifaa vya chakula viwe vya bati au mfupa mgumu, ambavyo ni sahani moja, bakuli moja, kikombe kimoja, na kijiko kimoja (vyombo vya plastiki haviruhusiwi). Tochi, Mwamvuli, Galoni la kuhifadhia maji ya kunywa na ndoo ya kuogea. **NB:** Vyombo vya chakula, ndoo ya kuogea, daftari, kalamu, Rimu ya karatasi, Tochi na Mwamvuli vinauzwa katika maduka yaliyopo karibu na chuo. Aidha, unatakiwa kuwa na fedha za kutosha kwa ajili ya matumizi yako binafsi.

6. ULIPAJI WA ADA NA MICHANGO

Unapofika chuoni utatakiwa kukabidhi risiti mbili za malipo ya Ada na Michango kama ilivyofafanuliwa hapa chini;

Na	**AINA YA MCHANGO**	**KIASI KWA MWAKA**
1.	Ada ya Mafunzo	450,000/=
2.	Serikali ya Wanachuo	5, 000
3.	Huduma ya kwanza	10,000
4.	Usafi na mazingira	20,000
5.	Kukodisha godoro	10,000
6.	Usajili na Kitambulisho kwa wanachuo wa mwaka wa kwanza tu	20,000
7.	Michezo	30,000
8.	Ulinzi	30,000
9.	Ukarabati	25,000
JUMLA		**600,000**

Piga simu namba **+255755489475 au +255653245339, +255752880668,** ili kuomba **Control Number** ya kulipa benki **Ada ya Tsh450,000.** Fedha ya **Michango Tsh 150,000** kwa mwaka ilipwe katika benki ya NMB kwenye akaunti namba **22001100005,** jina la akaunti ni **Mhonda Teachers' College. N.B: (i)** Pesa taslimu **haipokelewi** chuoni. (**ii**) Malipo ya Ada na Michango yote hapo juu yanaweza kulipwa katika **awamu mbili** kwa mwaka**.** Aidha, fedha za matumizi binafsi ya mwanachuo zisiwekwe kwenye akaunti hiyo hapo juu kwani akaunti za serikali haziruhusiwi kuweka au kutoa fedha za matumizi binafsi ni vema mwanachuo akafungua akaunti yake binafsi.

7. UTHIBITISHO WA AFYA

Unapaswa kupimwa afya yako kabla ya kufika Chuoni na daktari yeyote wa Hospitali inayotambuliwa na Serikali. Iwapo utakuja bila uthibitisho wa daktari udhuru wowote hautapokelewa. Kama unatumia dawa maalum kulingana na maradhi yako uje na dawa zako. Chuo kinatoa huduma ya kwanza tu. Fomu ya kupimwa afya yako inapatikana kwenye tovuti ya chuo. Aidha, matibabu yoyote ya mwanachuo **yanagharimiwa na mzazi/mlezi**. Hivyo, mwanachuo anatakiwa aje na kadi yake ya Bima ya afya ya **NHIF au Tsh 50,400/=**.

8. CHAKULA

Chuo kinatoa Chakula lakini hakitoi chakula maalumu (**Special Diet**) kwa Mwanachuo yeyote.

9. SHUGHULI ZA NJE.

9.1. **Uzalishaji Mali**: Katika jitihada za kuendeleza Elimu ya kujitegemea, Chuo kina miradi mbalimbali inayoendeshwa na Wanachuo wenyewe. Kila Mwanachuo atapaswa kushiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji na ujenzi wa Taifa.

9.2. **Utunzaji wa Mazingira na Mali za Chuo**: Ufikapo Chuoni utagawiwa eneo la kutunza.

Ni matarajio yetu kwamba utatunza Majengo na Mazingira ya Chuo kulingana na maelekezo utakayopewa. Utawajibika kutunza mali ya umma utakayokabidhiwa na Chuo na ya kwako binafsi. Ukipoteza au kuharibu mali hiyo utalazimika kulipa.

10. SHERIA ZA CHUO

Utapaswa kufuata sheria, kanuni na taratibu zote za chuo kwa muda wote wa mafunzo, sheria hizo zinapatikana kwenye tovuti ya chuo ambayo ni **www.mhondatc.ac.tz.**

11. KUFUNGUA CHUO

11.1. Chuo kitafunguliwa rasmi tarehe **17/07/2023**.

11.2. Masomo yataanza rasmi tarehe **24/07/2023**. Hakikisha unaingia darasani kwa tarehe hiyo bila kukosa.

11.3. Mwisho wa kuripoti chuoni ni tarehe **31/07/2023**.

12. MOTTO WA CHUO

ELIMU ILETE USAWA WA BINADAMU

13. DIRA YA CHUO

Kuandaa Walimu Walio Bora, Wazalendo, Wenye Maadili, Wanaojali Jinsia, Haki na Wajibu, Kwa Kutumia Miundo Mbinu Thabiti Kwa Kuzingatia Mahitaji ya Jamii na Taifa

14. DHAMIRA YA CHUO

“Chuo kuwa Chachu ya Mabadiliko Chanya Kitaaluma, Kitaalam na Kimaadili kwa Kuchochoea Ubunifu, Udadisi, Utafiti na Kuthubutu Kutenda ili Kuiwezesha Jamii Kukabiliana na Changamoto Zitokanazo na Mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia katika Kuleta Mabadiliko Endelevu

JUMUIYA YA CHUO INAKUKARIBISHA CHUONI MHONDA

KARIBU SANA CHUO CHA UALIMU MHONDA

Lucas W. Samwel

MKUU WA CHUO

GOVERNMENT OF TANZANIA REQUEST

FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A: **From: Mhonda Teachers' College**

To the Medical Officer

……

……

……

Mr./Mrs/Miss ……..(Name in full)

Please examine the above named as to his/her Physical and Mental fitness for a full time Teacher Training Course. The examination should include the following categories [I-II each category or sub category of which will render the applicant ineligible in case of a defect. Primary/Category IV] will aso render a girl candidate ineligible for the course:

I. [a] Eye –sight [b] Hearing [c] Limbs [d] Speech [e] Venereal disease [f] Leprosy [g] Epilepsy

II. Neuross III. Pregnancy (IV) Other serious diseases like TB, HIV ,…….……

MEDICAL CERTIFICATE

PART B: (To be completed by a government medical officer)

I have examined the above named and consider that he/she is physical fit unfit and mentally fit/unfit for a full time teacher training course.

I.[a] Eye-sight……... [b] Hearing…….…… [c] Limbs……... [d] Speech……...……

[e] Venereal disease……... [f] Leprosy……. [g] Epilepsy……..……

II. Nouroses …….

III. Serious diseased……..

IV. Prefinancy ….……

Name……..Signature…….. Date……..

Designation …….....Station ……..

Official Stamp: